# MATESO YAKO BWANA WANGU.

**PETER AMMI**
**KIBOSHO SEMINARI**
**13 March. 2022**

KWARESMA




1. Ee Yesu wangu mwema unateseka kwa ajili ya dhambi zangu*
   Unifundishe niache dhambi za uregevu, nikurudie wewe.

2. Ee Yesu umebeba msalaba huo mzito*
   unakubali kuelemewa kwa ajili ya kutuokoa sisi wanadamu.

3. Ee Yesu wewe umejinyenyekeza mpaka kufa*
   Unifundishe moyo wa sadaka na kujitoa kwa ajili ya wengine.

4. Ee Yesu ulianguka chini ya msalaba kisha ukasimama*
   Usiniache katika tamaa nikianguka dhambini,
   bali nisimame mara moja nikufuate.

5. Ee Yesu unijalie neema ya kuepuka nafasi za dhambi*
   na visa vyote vyenye kunikwaza na kunirudisha dhambini.

*p*